

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1  
Fax Nam. + 255 24 2230215  
Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)



SANDUKU LA BARUA 902,  
ZANZIBAR  
Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

## **TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA MBILI WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 26 NOVEMBA, 2018**

Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 28 Novemba, 2018, saa 3:00 asubuhi.

### **A: SHUGHULI ZA BARAZA**

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

#### **1. Maswali na Majibu.**

Maswali **123** yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

#### **2. Miswada ya Sheria**

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa Septemba, 2018 itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- ii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya Mwaka 2004 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.
- iii) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar

ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3. Taarifa ya Serikali kuhusu Hoja ya Mjumbe ya kutoa Azimio la kuitaka Serikali kuja na Mkakati unaotekelezeka kwa kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa zao la Mwani.
4. Hoja ya Mjumbe kuhusu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka viti Maalum vya Wanawake kufaidika na fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo.
5. Hoja ya Mjumbe kuhusu kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa miradi Zanzibar.

**(Raya Issa Msellem)**  
**KATIBU**  
**BARAZA LA WAWAKILISHI**  
**ZANZIBAR**

**Tarehe 26 Novemba, 2018**